# MUUNDO WA MTIHANI WA SOMO LA KISWAHILI

## 1.0 UTANGULIZI

Muundo wa mtihani huu umetayarishwa kuwaongoza watahini jinsi ya kutunga maswali ya mtihani. Muundo huu unajumuisha mada zilizomo katika muhtasari wa mwaka 2022 kuanzia Darasa la V, VI na VII. Malengo ya jumla, ujuzi na maudhui ya mtihani yaliyomo humo yanatokana na muhtasari wa somo la Kiswahili uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA-2022) Zanzibar.

## 2.0 MATOKEO YA JUMLA

Ujuzi wa jumla utakaopimwa katika mtihani wa Kiswahili utajumuisha uwezo wa mwanafunzi kuweza: -

2.1 Kuwasiliana kwa lunga ya Kiswahili kwa njia ya mazungumzo na maandishi.

2.2 Kusikiliza na kusoma Habari Pamoja na kuzifahamu.

2.3 Kuandika matini ndogo ndogo kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

## 3.0 MALENGO YA JUMLA

Malengo ya jumla ya mtihani wa Kiswahili ni kupima yafuatayo: -

3.1 Kusoma na kuandika matini za Kiswahili kwa usahihi na ufasaha.

3.2 Kusoma vitabu na machapisho mengine katika maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kujipatia maarifa mapya na burudani.

3.3 Kufahamu mbinu za mawasiliano katika muktadha na nyakati tofauti.

3.4 Kupata stadi za usomaji na uandishi sahihi katika Kiswahili.

3.5 Kuelewa utungaji, ubunifu, na uandishi wa kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili kwa kuzingatia lugha ya kisanii.

3.6 Kutumia vipengele vya msingi vya sarufi ya Kiswahili katika kuzungumza na kuandika.

3.7 Kutumia lahaja za Kiswahili za Zanzibar kama sehemu ya kuimarisha lugha na mawasiliano.

3.8 Kuelewa uchambuzi wa vipengele tofauti vya Kiswahili sanifu.

3.9 Kuelewa uhusiano kati ya maneno na nambari katika lugha ya Kiswahili.

3.10 Kutumia makamusi ya lugha katika kutatua matatizo ya kimsamiati na kimaana.

3.11 Kuthamini, kufurahia na kujivunia Kiswahili kama ni lugha ya Taifa na Kimataifa.

3.12 Kuwa na maarifa ya msingi ya Fasihi Andishi.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Kutakuwa na mtihani mmoja wenye muda wa saa mbili na nusu (2.30) na kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu utafanywa kwa muda wa saa tatu (3:00). Muundo huu unaojumuisha maswali kumi na mbili (12) yaliyogawika katika sehemu nne (4) A, B, C na D. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali (9). Maswali yote ya sehemu A, manne (4) kutoka sehemu B, mawli (2) kutoka sehemu C na moja (1) kutoka sehemu D. Mtihani huu utakuwa na alama 100.

### 4.1 **SEHEMU A: UFAHAMU: (Alama 15)**

Sehemu hii itakuwa na maswali mawili (1 – 2). Swali la kwanza litakuwa la kusoma kwa ufahamu lenye vifungu vitano (5) vya maswali. Kila kifungu kitakuwa na alama mbili (2). Swali la pili litakuwa la ufupisho lenye alama tano (5).

### 4.2 **SEHEMU B : SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** : **(Alama 40)**

Sehemu hii itakuwa na maswali matano (3 – 7) ya majibu mafupi. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali manne (4). Kila swali litakuwa na alama kumi (10), ambayo yatahusu sarufi na matumizi ya lugha.

### 4.3 **SEHEMU C : FASIHI NA UTAMADUNI WA MSWAHILI : (Alama 30)**

Sehemu hii itakuwa na maswali matatu (8-10). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali mawili (2). Kila swali litakuwa na alama kumi na tano (15), ambayo yatahusu Fasihi na Utamaduni wa Mswahili.

### 4.4 **SEHEMU D : UTUNGAJI** : **(Alama 15)**

Sehemu hii itakuwa na maswali mawili (2) yanayohusu Utungaji. Mtahiniwa atatakiwa kujibu swali moja (01) litakalokuwa na alama kumi na tano (15).

## 5.0 MADA ZITAKAZOTAHINIWA

5.1 Usomaji
5.2 Sarufi
5.3 Matumizi ya Lugha
5.4 Fasihi simulizi
5.5 Fasihi andishi
5.6 Utamaduni wa Mswahili
5.7 Utungaji

**JADUWELI LA UTAHINI**

| | | Nyanja za utambuzi zitakazopimwa | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mada** | **kukumbuka** | **kufahamu** | **kutumia** | **kuchambua** | **kutathmini** | **kuunda** | **Idadi ya maswali** | **Asilimia kwa kila mada** |
| 1. | USOMAJI | | | | | | | 3 | 7.96 |
| 2. | MATUMIZI YA LUGHA NA MAWASILIANO | | | | | | | 5 | 15.44 |
| 3. | FASIHI SIMULIZI | | | | | | | 3 | 7.80 |
| 4. | FASIHI ANDISHI | | | | | | | 1 | 4.37 |
| 5. | SARUFI | | | | | | | 10 | 29.17 |
| 6. | UANDISHI | | | | | | | 8 | 24.49 |
| 7. | UTAMADUNI WA MSWAHILI | | | | | | | 4 | 10.76 |
| **Idadi ya maswali kwa kila nyanja** | | | | | | | | **34** | |
| **Asilimia ya maswali kwa kila nyanja.** | | | | | | | | | **100** |